

Ni asubuhi yenye kupendeza katika jiji la Dar es salaam Patrick alikuwa na miadi yakukutana na profesa mbobezi katika masuala ya uchunguzi. "kwahiyo prof nitaingia jengo gani?" anamuuliza kwa njia ya simu huku akitembea.

Patrick alikuwa kijana aliyekuwa amesoma nakujikita katika habari za uchunguzi "ukifika ulizia jengo la utawala nakisha pandisha juu" anamuelekeza profesa "sawa nimesha fika" mwendo wake ulikuwa niwaharaka alikuwa kijana mwembamba na mpole asiye penda kuongea zaidi kusikiliza.

Punde anafika mbele yake katika lango la kuingia ilikupandisha ngazi hadi kufika ofisi ya profesa anakutana na mlinzi "unaenda ofisi gani?" kwakuwa Patrick alikuwa anajiamini anajibu,

"kwa prof Mtabale" mlinzi kwa jinsi Patrick alivyokuwa anajieleza kwa haraka anamkubalia "panda gorofa ya tatu chumba namba 30 upande wa kulia" patirck anapandisha ngazi kwa kadili alivyokuwa amelekezwa na mlinzi lakini na profesa ambae alikuwa rafiki yake:

"habari yako kijana" alimsemesha profesa,

"salama mzee" anamjibu huku akiendelea kusoma gazeti la kingereza la **THE MONOTOR** "kwanini unasoma gazeti hili wakati sio kawaida ya vijana wengi wa kitanzania?" aliuliza huku akishangaa kwasababu utamaduni wa usomaji hasa wa vitu vigumu na kipembuzi kwa vijana wakitanzania ilikuwa sio tabia yao.

"Ninapenda kusoma ili akili yangu itanuke" wakati patirck anapandisha ngazi anakumbuka siku ya kwanza walipokutana na profesa nakuanza mazungumzo yao,

Profesa alikuwa na shauku yakutaka kuonana kwa mala yapili na Patrick "huyu kijana nahisi leo nitazungumza naye vitu vingi" anawaza akilini kisha anamfuata mtu wa mapokezi pale ofisini kwake.

"naomba uniandalie kahawa tafadhari kwasababu nitakuwa na mazungumzo marefu na huyu mgeni wangu" mezani kwake kulikuwa na vitabu vingi mala baada yakutoka kuongea na secretary wake gafla anasikia mlango ukiwa una sukumwa.

"karibu" anasema secretary huku akisimama Patrick anaingia huku akijifuta jasho usoni kutokana nakupandisha ngazi "nina shida yakuonana na profesa" secretary kwasababu alisha pokea taarifa muda anamruhusu Patrick kuingia moja kwa moja ndani,

Mala wanapokutana kwa mala nyingine ya pili walikuwa niwenye furaha wote wawili "karibu patrick" aliongea huku akimnyooshea mkono mmoja "asante profesa" anaushika mkono kwa namna ya upendo na heshima kubwa kwa profesa.

kwanza akiwa mtu ambaye amemzidi umli pili akiwa ni mtu ambae amemzidi elimu na ujuzi wa mambo mengi Patrick aliamini hivyo na ndio sababu zilizomfanya kutoa heshima kubwa kwa profesa,

"karibu kiti" alisema profesa wanakaa sehemu ambayo profesa aliiweka maalumu kwaajili ya kukaa na wageni kuzungumza.

"nilipendekeza uje hapa ofisini kwasababu kuna vitu vingine tukiongea nitakuwa nakuonyesha" Patrick kwake ilikuwa hakuna kitu ambacho angeweza kupinga kutokana na profesa alichokuwa anaongea,

"Ndio prof ulisema vyuoni kuna wahadhiri wasio waadilifu ulikuwa na maana gani?" anamuuliza huku akiweka umakini kumsikiliza "kuna vitu vingi kwa wahadhiri

rushwa ya ngono, lakini hata rushwa ya kifedha" Patrick alikuwa makini "mazingira yapi ambayo yanasababisha hizo rushwa?"

"kuna muhadhiri anahitaji binti lakini hana njia yakumpata njia yake nyepesi sio kumtongoza, bali nikumkamata katika somo lake" Patrick anaonyesha kama ni suala geni kwake kulisikia.

"Aisee!" inamstajabisha,